REPUBLIC OF KENYA

PBORA
Public Benefit Organizations Regulatory Authority

# HATI YA UTOAJI HUDUMA

| HUDUMA | YANAYOHITAJIKA KWA MTEJA | MUDA WA KUJIBU | ADA YA USINDIKAJI (KSH.) |
|---|---|---|---|
| **HUDUMA ZA KABLA YA KUSAJILIWA** | | | |
| Utafutaji/Uhifadhi au Uongezaji wa Muda wa Uhifadhi wa Jina | i. Ombi la utafutaji/uhifadhi au uongezaji wa muda wa uhifadhi wa jina kwenye tofuti ya https://pbora.ecitizen.go.ke | Nusu ya siku | 1,000 |
| Usajili wa Shirika la Manufaa ya Umma | i. Fomu ya maombi (Fomu 1) iliyojazwa ipasavyo<br>ii. Thibitisho la uhifadhi wa jina<br>iii. Maelezo ya angalau wakurugenzi watano wa baraza linaloongoza (angalau theluthi moja ya wakurugenzi waliopendekezwa LAZIMA wawe raia na wakazi wa Kenya)<br>iv. Picha ya hivi karibuni, ya ukubwa wa pasipoti, yenye rangi (kwenye mandharinyuma nyeupe, inchi 2x2) ya kila mmoja wa wakurugenzi waliopendekezwa<br>v. Vyeti halali vya mwenendo mwema kwa raia wa Kenya au vyeti sawa vilivyohakikiwa na wakili kwa wageni wasio wakazi.<br>vi. Nakala ya katiba ya shirika iliyotiwa sahihi kikamilifu<br>vii. Kumbukumbu za mkutano (kuwasilishwa ndani ya siku 30) zinazoidhinisha usajili wa shirika kama shirika la manufaa ya umma<br>viii. Bajeti pendekezi ya mwaka mmoja<br>ix. Cheti cha usajili cha kigeni kilichohakikiwa na wakili (kwa mashirika ya kimataifa)<br>x. Idhini, kutoka kwa shirika-zazi, ya kujiandikisha nchini Kenya (kwa mashirika ya kimataifa) | Siku 60 | 25,000 kwa Mashirika ya Kitaifa<br>45,000 kwa Mashirika ya Kimataifa |
| Kukabidhiwa Hali ya Shirika la Manufaa ya Umma kwa Shirika lililopo tayari Kenya | i. Fomu 3 iliyojazwa ipasavyo ikiwa na maelezo ya angalau wakurugenzi watatu, angalau mmoja wa wakurugenzi waliopendekezwa LAZIMA awe raia na mkazi wa Kenya<br>ii. Picha ya hivi karibuni, ya ukubwa wa pasipoti, yenye rangi (kwenye mandharinyuma nyeupe, inchi 2x2) ya kila mmoja wa wakurugenzi waliopendekezwa<br>iii. Vyeti halali vya mwenendo mwema kwa raia wa Kenya au vyeti sawa vilivyohakikiwa na wakili kwa wageni wasio wakazi.<br>iv. Cheti halali cha usajili kutoka kwa shirika husika la usajili<br>v. Thibitisho la hali njema kwa shirika husika la usajili<br>vi. Hati inayounda shirika (lazima ijumuishe lengo la faida ya umma)<br>vii. Kumbukumbu za mkutano, zilizotiwa sahihi ipasavyo, uliopendekeza kukabidhiwa hali ya shirika la manufaa ya umma<br>viii. Ripoti ya hesabu zilizokaguliwa za miaka mitatu iliyopita kabla ya tarehe ya maombi | Siku 60 | 20,000 |
| Msamaha wa Usajili kwa Shirika la Kimataifa | i. Fomu 6 iliyojazwa ipasavyo<br>ii. Thibitisho la uhifadhi wa jina<br>iii. Maelezo ya wakurugenzi wa shirika<br>iv. Maelezo ya wakala wa shirika, yakiwemo picha ya ukubwa wa pasipoti na cheti cha mwenendo mwema (Wakala lazima awe Mkenya)<br>v. Picha ya hivi karibuni, ya ukubwa wa pasipoti, yenye rangi (kwenye mandharinyuma nyeupe, inchi 2x2) ya kila mmoja wa wakurugenzi<br>vi. Vyeti vya mwenendo mwema vya wagurugenzi vilivyohakikiwa na wakili<br>vii. Nakala ya cheti cha usajili cha shirika-zazi iliyohakikiwa na wakili<br>viii. Kumbukumbu za mkutano, zilizotiwa sahihi ipasavyo, kutoka kwa Bodi ya shirika zikibainisha uamuzi wa kutafuta kibali cha kufanya kazi kama shirika la manufaa ya umma lililosamehewa usajili | Siku 60 | 75,000 |
| **HUDUMA ZA BAADA YA KUSAJILIWA** | | | |
| Kutambuliwa kwa Jukwaa la Mashirika ya Manufaa ya Umma | i. Fomu 11 iliyojazwa ipasavyo<br>ii. Thibitisho la uhifadhi wa jina lililopendekezwa<br>iii. Hati zinazounda jukwaa<br>iv. Kumbukumbu za mkutano, zikiwa na azimio la kuunda jukwaa, zilizotiwa sahihi na maafisa wa wanachama wanaoliunda<br>v. Kumbukumbu za mkutano, zilizotiwa sahihi ipasavyo, za kila shirika linalounda jukwaa ukiliruhusu kujiunga na jukwaa<br>vi. Maelezo ya maafisa waliopendekezwa<br>vii. Vyeti vya usajili vya kila shirika linalounda jukwaa (angalau mashirika kumi)<br>viii. Kanuni za maadili na viwango vya nidhamu kwa jukwaa | Siku 60 | 10,000 |
| Kutambuliwa kwa Shirikisho la Majukwaa | i. Fomu 11 iliyojazwa ipasavyo<br>ii. Thibitisho la kuhifadhi jina lililopendekezwa<br>iii. Hati zinazounda shirikisho<br>iv. Kumbukumbu za mkutano, zilizo na azimio la kuunda shirikisho, zilizotiwa sahihi na maafisa wa wanachama wanaoliunda<br>v. Kumbukumbu za mkutano, zilizotiwa sahihi ipasavyo, wa kila jukwaa unaoliruhusu kujiunga na shirikisho<br>vi. Maelezo ya maafisa waliopendekezwa<br>vii. Vibali vya kutambuliwa kwa kila jukwaa linalounda shirikisho (angalau majukwaa matano)<br>viii. Kanuni za maadili kwa wanachama wa shirikisho | Siku 60 | 20,000 |
| Marekebisho ya Katiba ya Shirika | i. Fomu 14 iliyojazwa ipasavyo<br>ii. Kumbukumbu za mkutano unaoidhinisha marekebisho, zilizotiwa sahihi na maafisa wa shirika, zikibainisha mabadiliko na sababu za mabadiliko hayo<br>iii. Nakala ya katiba iliyorekebishwa | Siku 7 | 4,000 |
| Mabadiliko/Kuongezwa kwa Maafisa wa Shirika | i. Fomu 14 iliyojaazwa ipasavyo<br>ii. Kumbukumbu za mkutano, unaoidhinisha mabadiliko, zilizotiwa sahihi na maafisa wa shirika, zikieleza sababu za mabadiliko | Siku 14 | 4,000 |
| Mabadiliko ya Mipango ya Benki ya Shirika | i. Fomu 14 iliyojazwa ipasavyo<br>ii. Kumbukumbu za mkutano ulioidhinisha mabadiliko, zikiwa zimetiwa sahihi ipasavyo na maafisa wa shirika, zikieleza sababu za mabadiliko | Siku 1 | 4,000 |
| Mabadiliko ya jina la Shirika | i. Fomu 15 iliyojazwa ipasavyo<br>ii. Thibitisho la kuhifadhi jina jipya<br>iii. Kumbukumbu za mkutano, zikiwa na azimio la kubadilisha jina, zilizotiwa sahihi na Mkurugenzi wa shirika zikibainisha sababu za kubadili jina<br>iv. Nakala ya tangazo katika gazeti lenye usambazaji wa kitaifa likijulisha umma kuhusu mabadiliko ya jina<br>v. Thibitisho la idhini ya mabadiliko ya jina kutoka kwa mdhibiti mkuu (kwa mashirika yaliloyosamehewa usajili au mashirika yaliyopewa hali ya Shirika la Manufaa ya Umma) lisilozidi siku 30 | Siku 7 | 15,000 kwa Mashirika ya Kitaifa<br>27,500 kwa Mashirika ya Kimataifa |
| Mabadiliko makubwa katika Majukwaa/Mashirikisho (Maafisa, uanachama, katiba/hati zinazounda, mipango ya benki) | i. Fomu 14 iliyojazwa ipasavyo<br>ii. Kumbukumbu za mkutano unaoidhinisha mabadiliko, zilizotiwa sahihi ipasavyo na maafisa wa jukwaa/shirikisho, pamoja na sababu za mabadiliko<br>iii. Kumbukumbu za mkutano wa shirika/jukwaa zikiwa na azimio la kujiunga na/kuondoka kwenye jukwaa/shirikisho, zilizotiwa sahihi na maafisa wa mashirika yanayounda<br>iv. Nakala ya katiba/hati zinazounda zilizorekebishwa (ile inatakikana) | Siku 30 | 5,000 |
| Mabadiliko ya Wakala Aliyeidhinishwa | i. Ombi la mabadiliko ya wakala<br>ii. Kumbukumbu za mkutano ulioidhinisha mabadiliko hayo, zilizotiwa sahihi ipasavyo na viongozi wa shirika, zikieleza sababu za mabadiliko hayo<br>iii. Maelezo ya wakala aliyeidhinishwa anayeingia | Siku 14 | 20,000 |
| Nakala za Nyaraka Zilizohakikiwa | i. Ombi linalobainisha nyaraka zinazohitajika kuhakikiwa na sababu | Siku 1 | 4,000 |
| Uhakiki wa Nyaraka Nyingine | i. Ombi la uhakiki<br>ii. Uwasilishaji wa nyaraka, pamoja na thibitisho la malipo, kwa Mamlaka kwa ajili ya uhakiki | Ndani ya dakika 30 ya kuwasilisha nyaraka. | 4,000 |
| Upekuzi Rasmi wa Jalada | i. Ombi la upekuzi wa jalada na sababu ya upekuzi | Siku 1 | 4,000 |
| Uwasilishaji wa Ripoti za Mwaka | i. Fomu 13 iliyojazwa ipasavyo<br>ii. Lazima ripoti ziwasilishwe ndani ya miezi 6 kutoka mwisho wa mwaka wa kifedha<br>iii. Hesabu zilizokaguliwa | Siku 2 | 2,000 |
| Kuvunjwa kwa Hiari kwa Shirika | i. Ilani kwa Mamlaka, kuhusu kuvunjwa kwa shirika (ilani itolewe ndani ya siku 14 baada ya azimio la kuvunjwa na lazima itiwe sahihi na angalau theluthi mbili ya wanachama wa Bodi/wakurugenzi)<br>ii. Kumbukumbu za mkutano ulioidhinisha kuvunjwa kwa shirika, pamoja na sababu<br>iii. Orodha ya mali za shirika na mpango wa uhamishaji wa mali hizo kwa shirika lingine lenye malengo sawa<br>Mamlaka inaweza kufanya uamuzi kuhusu ugawanyi wa mali | Siku 21 | Bure |
| Marejesho Baada ya Kusimamishwa | i. Fomu 10 iliyojazwa ipasavyo | Siku 14 | Bure |
| Marejesho Baada ya Kughairiwa Cheti | i. Fomu 10 iliyojazwa ipasavyo | Siku 14 | Bure |

**KUMBUKA: Huduma zote hutolewa mtandaoni kupitia tovuti ya eCitizen ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mashirika ya Manufaa ya Umma kwenye https://pbora.ecitizen.go.ke/ . Ada za usindikaji zilizotajwa katika hati ya utoaji huduma hazijumuishi ada za urahisi zinazotozwa na mtandao wa eCitizen.**

## Huduma Bora ni Haki Yako!

**MKURUGENZI / AFISA MTENDAJI MKUU**
**MAMLAKA YA UDHIBITI WA MASHIRIKA YA MANUFAA YA UMMA**
Jengo la Cooperative Bank, Ghorofa ya 15
Barabara ya Haile Selassie
S.L.P. 44617 - 00100, Nairobi - Kenya
Simu: +254 (0) 111 053 310
(020) 221 40444/221 4813/221 3938
Baruapepe: info@pbora.go.ke/ed@pbora.go.ke
Wavuti: www.pbora.go.ke

**KATIBU WA TUME**
**TUME YA HAKI YA UTAWALA**
(Ofisi ya Mpatanishi wa Malalamishi ya Umma)
Jengo la West End Towers, Ghorofa ya 2
S.L.P. 20414 - 00200, Nairobi - Kenya
Simu: +254 (020) 222 70000
Baruapepe: complain@ombudsman.go.ke

@PBO_RA

@PBORADigital